# HALMASHAURI YA JIJI LA MWANZA

**BARUA ZOTE ZIANDIKWE KWA MKURUGENZI WA JIJI**

SIMU MKURUGENZI : **225 028 501375**
OFISI ZOTE**: 40334**
FAX: **255 028 500785**

S.L.P. 1333
**MWANZA.**

20.04.2017

# T A N G A Z O

**ZABUNI YA UWAKILISHI KUENDESHA MAENEO YA WAZI AU BUSTANI ZA JIJI (DEVELOPMENT AND MAINTANANCE OF CITY OPEN SPACES AND PARKS) KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018**

**ZABUNI NA. LGA/089/2017-2018/NC/04**

1. Halmashauri ya Jiji la Mwanza inapenda kuwaalika watu binafsi, makampuni, Ushirika, Taasisi au vikundi vya watu vilivyosajiliwa kisheria wenye nia, uwezo na uzoefu wa kuwakilisha kazi hiyo kutuma maombi yao kwa zabuni hii kuendesha maeneo ya wazi au bustani za Jiji (Development and maintenance of City Open Spaces and Parks) kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

**FUNGU 1. ROCK BEACH (MWANZA BELLEVUE). ZABUNI NA. LGA/089/2017-2018/NC/04/01**
Ni bustani iliyopo eneo la Kivuko cha Kamanga kando kando ya barabara ya Nasser ndani yake likiwemo jiwe maarufu la Bismark Rock na Hotel ya Rock Beach – Yun Long.

**FUNGU 2. CUSTOM PARK. ZABUNI NA. LGA/089/2017-2018/NC/04/02**
Bustani hii inapatikana katikati ya Bandari ya Kaskazini na Kivuko cha Kamanga, kwa upande wake wa magharibi ni barabara inayounganisha mwisho wa barabara ya Posta na Bandari ya Kaskazini/Polisi kati. Kwa upande wa juu (Mashariki) bustani imepakana na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mwanza.

**FUNGU 3. SERENGETI PARK. ZABUNI NA. LGA/089/2017-2018/NC/04/03**
Bustani hii inapatikana katikati ya barabara ya Mkanyenye na Rufiji katika eneo lenye makazi mengi.

**FUNGU 4. NYEGEZI TERMINAL PARK ZABUNI NA. LGA/089/2017-2018/NC/04/04**
Bustani hii inapatikana katika eneo la Kituo Kikuu cha Mabasi cha Nyegezi, pembezoni mwa barabara ya Kenyatta (barabara ya Mwanza – Shinyanga). Kwa upande wa kusini mpaka ni barabara ya kuingia stendi ya Nyegezi na kwa upande wa Kaskazini mpaka ni barabara ya kutoka Kituo cha Nyegezi. Kwa sasa bustani hii ipo katika eneo muhimu liitwalo lango kuu la kuingia na kutoka Mwanza kwa njia ya barabara.

**FUNGU 5. CAPRI POINT PARK ZABUNI NA. LGA/089/2017-2018/NC/04/05**
Bustani hii ndogo iko Kata ya Nyamagana. Upande wa Mashariki na Kaskazini ya eneo hili la bustani imepakana na Jengo la Hotel linalojengwa na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), na upande wa kusini imepakana na Chuo cha Bank Kuu. Upande wa Magharibi imepakana na makazi.

**FUNGU 6. BUSTANI YA MAKUTANO YA BARABARA YA PAMBA NA KENYATTA (PAMBA/KENYATTA TRIANGLE) ZABUNI NA. LGA/089/2017-2018/NC/04/06**

Hii ni bustani/eneo la wazi dogo lililopo mwisho wa barabara ya Pamba katika makutano na barabara ya Kenyatta. Ni kipande cha ardhi chenye kufanana na umbo la pembe tatu linalopakana na Kituo cha Mafuta kwa upande wa Kaskazini, na kwa juu upande wa Mashariki ni barabara ya Pamba na chini ni barabara ya Kenyatta.

2. Maombi yote ya zabuni yazingatie masharti yafuatayo
   i) Nyaraka za zabuni kwa lugha ya Kiswahili zinapatikana kwa Katibu wa Bodi baada ya kulipia ada ya maombi ya **Tshs. 100,000/=** (Ambayo haitarudishwa)
   ii) Ombi la zabuni liwe na jina na anuani halisi ya mwombaji, aidha aonyeshe mahali ofisi zake zilipo au anapoweza kupatikana (physical address).
   iii) Mwombaji aonyeshe mchanganuo wa matokeo ya mapato anayotarajia kukusanya, matumizi anayotarajia kuyafanya na kiasi atakachoilipa Halmashauri kwa mwezi.
   iv) Zingatia kuwa form ya maombi ya Zabuni inajazwa na kusainiwa na mwenye uhalali wa kisheria (power of Attorney) katika zabuni hii kama ni kampuni
   v) Mwombaji wa zabuni endapo atachaguliwa atahitajika kuleta dhamana ya kufanya kazi (Performance Bond), kwa njia ya Banker`s cheque kutoka bank husika na kiasi cha malipo ya miezi mitatu ya kiasi alichoahidi kuilipa halmashauri kwa wazabuni watakaoshinda zabuni.
   vi) Mwombaji aonyeshe vifaa alivyonavyo, idadi ya wafanyakazi na uzoefu wao.
   vii) Mwombaji awasilishe zabuni Original na nakala mbili (2) endapo maelezo ya original na nakala yatatofautiana Original ndio itatumika kwenye tathmini.
   viii) Zabuni ijazwe vizuri, iwekwe kwenye bahasha isiyo na maandishi yoyote (Plain) na juu ya bahasha iandikwe, namba ya zabuni, kazi inayoombwa, Original & Copy, Anuani ya mkurugenzi bila kuwekwa alama yoyote.
   ix) Dhamana ya zabuni: Dhamana ya zabuni (Bid Security) italetwa kwa njia ya Banker’s Cheque ambayo itakuwa ni asilimia mbili (2%) ya marejesho ya miezi mitatu ya kiasi alichoahidi mzabuni.
3. Mwombaji atakayeshindwa masharti haya atakuwa amejiondoa mwenyewe kwenye mchakato mzima wa zabuni.
4. Zabuni zitawasilishwa kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Mwanza.
5. Mwisho wa kupokea zabuni ni **saa nne (4) kamili asubuhi** (saa ya Afrika Mashariki) ya tarehe **12/05/2017 siku ya Ijumaa** katika **ofisi ya Mkurugenzi wa Jiji zilizopo Halmashauri ya Jiji la Mwanza.** Waombaji au wawakilishi wa waombaji wanaalikwa kushuhudia ufunguzi. Ufunguzi utafanywa mara tu baada ya saa ya mwisho ya kupokea zabuni mbele ya waombaji au wawakilishi wa waombaji waliochagua kuhudhuria ufunguzi huo utakaofanyika katika Ukumbi Mkubwa katika ofisi za Halmashauri ya Jiji la Mwanza.

   Anuani ya kutuma zabuni hizo ni:-

   MKURUGENZI HALMASHAURI YA JIJI LA MWANZA

   S.L.P. 1333, **MWANZA**
6. Zabuni ambazo zitachelewa kwa muda uliopangwa na zabuni zitakazotumwa kwa mtandao (e-mail) hazitapokelewa.

**KIOMONI KIBURWA KIBAMBA**
**MKURUGENZI WA JIJI**
**MWANZA.**